**HOTUBA YA MKUU WA MKOA KWENYE UFUNGUZI WA MKUTANO WA WADAU WA CHANJO YA SARATANI YA MLANGO WA KIZAZI TAREHE 19 APRIL, 2018.**

- Mwakilishi kutoka TAMISEMI,
- Mwakilishi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto,
- Wawakilishi wa wadau wa Maendeleo wote mliopo hapa,
- Katibu Tawala Mkoa
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,
- Mheshimiwa Meya na Wenyeviti wa Halmashauri,
- Wakurugenzi wa Manispaa na Wakurugenzi Watendajiwa wa Halmashauri za Wilaya,
- Waganga Wakuu wa Wilaya,
- Waratibu wa Elimu waWilaya,
- Wafanyakazi wa Sekta ya Afya na Elimu,
- Waandishi wa Habari wote mliopo hapa,

Habari ya Asubuhi.

**Ndugu Wadau wa Chanjo,**

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha sote kuwa hapa siku ya leo. Pili napenda kuwashukuru kwa kunialika kujumuika nanyi katika tukio hili muhimu la mkutano na wadau wa chanjo katika Mkoa wetu.Pia, nachukua fursa hii kuwapongeza wote ambao mmejumuika hapa na ushiriki wenu katika kikao kazi hiki muhimu.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na wadau wa chanjo Taifa, inaanzisha chanjo mpya ya kuwakinga wasichana dhidi yaugonjwa wa Saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana wenye umri wa miaka 14 kuanzia mwezi Aprili,2018 nchi nzima.

Lengo hasa la kuanzisha chanjo hii ni kuweza kuwakinga mabinti wetu kutokana na madhara makubwa yanayoweza kuwapata ambayo husababisha vifo vingi kwa wanawake, na hivyo kuweza kuboresha afya za jamii ya wanawake na watanzania kwa ujumla.

**Ndugu Wadau wa Chanjo,**

Nchini Tanzania, Saratani ya mlango wa kizazi niya kwanza kusababisha vifo. Takwimu kutokaTaasisi ya Ocean Road za mwaka **2016/17** zinaonesha kwamba Saratani ya mlango wa kizazi ndiyo inayoongoza kuwa na wagonjwa wengi kwa asilimia **32.8** na Saratani ya mlango wa kizazi huchangia asilimia **38** ya vifo vitokanavyo na Saratani.

Kwa Mkoa wa Lindi katika kipindi cha mwaka **2016/2017** jumla ya Wanawake **3002** waliweza kupimwa katika vituo vya kutolea huduma za Afya, kati yao waliogundulika viachanya (Dalili za awali za Saratani) **ni 36 (1%).** Waliopata huduma za awali (Cryotherapy) walikuwa ni **35 (97**%) na waliopata rufaa kwa ajili ya matibabu maalumu walikuwa ni **9 (25**%).

Katika kipindi cha mwaka **2017/2018** jumla ya Wanawake **1720** waliweza kupimwa katika vituo vya kutolea huduma za Afya, kati yao waliogundulika viachanya (Dalili za awali za Saratani) **ni 44 (2.6%).** Waliopata huduma za awali (Cryotherapy) walikuani **44 (100**%) na waliopata rufaa kwa ajili ya matibabu maalumu walikuwa ni **20 (1.2%).**

Kutokana na takwimu hizi inaonesha tatizo lipo, ili kukabiliana na tatizo hili hatua za kuongeza vituo vya uchunguzi zinatakiwa kuchukuliwa ili kupambana na kansa ya mlango wa kizazi.

Kwa sasa vituo vinavyotoa huduma ya uchunguzi wa kansa ya mlango wa kizazi ni 18, kati ya vituo 237.

Aidha takwimu zinaonesha kuwa ni asilimia **5** tu ya fedha za Saratani duniani zinazotolewa katika nchi za kusini mwa jangwa la sahara. Hivyo basi, hatuna budi kutumia vyanzo vyetu vya mapato vya ndani pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa huduma za chanjo.

Saratani ya mlango wa kizazi inachangiwa na vitu vingi ikiwemo kuanza kujamiiana katika umri mdogo, kuwa na wapenzi wengi, kuwa na ndoa za mitala, kuzaa watoto wengi na uvutaji wa sigara. Dalili za Saratani ya mlango wa kizazi mara nyingi hujitokeza ikiwa imeshasambaa mwilini.

Tunapaswa kujua namna ya kujikinga na Saratani ya mlango wa kizazi. Njia ya kwanza ni kupata chanjo ya kuzuia Saratani ya mlango wa kizazi, kutokufanya ngono katika umri mdogo, kuepuka kubeba mimba katika umri mdogo, kuwa na mwenzi mmoja mwaminifu, kutumia kondomu na kuepuka uvutaji wa sigara. Njiaya pili ni Kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini dalili za awali na kupata matibab ustahiki mapema. Na njia ya tatu ni kupata matibabu maalum kwa mtu ambaye tayari amepata Saratani ya mlango wa kizazi.

**Ndugu Wadau wa Chanjo,**

Uanzishwaji wa chanjo hii utahusisha pia Mkoa wetu. Walengwa wa chanjo hii kwa mwaka huu wa 2018 ni wasichana wote wanaotimiza miaka 14, ambao kwa mkoa wetu tunatarajia kuchanja wasichana wasiopungua **14,905.**

Napenda pia niwataarifu mkakati utakaotumika katika utoaji wa chanjo hii itatolewa katika utaratibu wa kawaida katika vituo vyetu vya kutolea huduma za Afya, baadhi ya shule zitakazochaguliwa, na baadhi ya maeneo katika jamii ambapo zitatolewa kwa njia za huduma za mkoba. Huduma hizi zitatolewa bila malipo katika vituo vya kutolea huduma za afya vya serikali na binafsi.

**Ndugu Wadau wa Chanjo,**

Ombi kubwa la serikali ni kuwaomba wadau wetu wote Taasisi ya Saratani Ocean Road. (ORCI) na kuwafariji mliopo hapa mtusaidie kupeleka ujumbe huu wa kuanzishwa kwa chanjo ya Saratani ya mlango wa kizazi kwa mabinti wa miaka 14 ili waweze kukingwa na madhara makubwa yanayoweza kuwapata hapo baadae ya kuugua kwa maumivu makali sana na hatimaye kifo. Wengi wetu tumetembelea wagonjwa waliopata madhara haya na kuona namna yanavyowatesa.

**Ndugu Wadau wa Chanjo**

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru OR-TAMISEMI, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na wadau mbalimbali waliochangia katika kufanikisha utoaji bora wa huduma za chanjo hapa nchini wakiwemo shirika la GAVI,Shirika la afya ulimwenguni WHO,Shirika la kuhudumia watoto UNICEF, CHAI, JSI, PATH, AMREF, JHPIEGO pamoja na wadau wengine kwa misaada yao ambayo imeweza kutufikisha hapa.

Naomba nihitimishe kwa kuwahakikishia wananchi kuwa chanjo zinazotolewa katika vituo vyetu ni salama, hutolewa na wataalamu wenye uzoefu mkubwa waliobobea katika fani hii kwa muda mrefu.

Mwisho napenda niwashukuru wote kwa kuweza kuhudhuhuria katika kikao hiki muhimu.

Baada ya kusema hayo naomba kutangaza kuwa kikao hiki cha wadau juu ya chanjo ya Saratani ya mlango wa kizazi kimefunguliwa rasmi.

***ASANTENI  SANA KWA KUNISIKILIZA;***